



# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 (0)22-2122722/3  
Nukushi: +255 (0)22-2130852  
Barua pepe: dg@nbs.go.tz  
Tovuti: www.nbs.go.tz

18 Barabara ya Kivukoni,  
S.L.P. 796,  
11992 - Dar es Salaam  
**TANZANIA.**



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb Na: NBS/S.40/21/521

## YALIYOJITOKEZA

Tarehe: 08 Februari, 2017

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KWA MWEZI JANUARI, 2017

### MAELEZO YA MBINU NA KANUNI ZA UKOKOTOAJI WA FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA

#### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za Bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na sampuli wakilishi ya kaya binafsi nchini Tanzania. Bei za bidhaa na huduma 278 zikiwa ni pamoja na bidhaa 97 za Vyakula na Vinywaji Baridi na 181 zisizo za Vyakula hukusanywa kila mwezi katika kila mkoa.

#### Mizania za Bidhaa na Huduma za Jamii na Kizio cha Bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 25 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijiji na yaliyotokana na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya binafsi wa mwaka 2011/12. Kizio cha bei kinachotumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa ni cha mwezi Desemba, 2015.

#### Makundi ya Bidhaa na Huduma za Jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi-vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

#### Namna ya Kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Kuna maboresho mengi yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric mean of Price Relatives" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo; matumizi ya mfumo ulioboreshwu wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Mbinu na kanuni ya Lowe Index Formula ambayo ni aina ya "Laspeyres Index Formula" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZeka HADI ASILIMIA 5.2

### Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Januari, 2017 (Des., 2015 = 100)

Na. .	KUNDI (MAIN GROUP)	Mizania (Weight)	Jan-16	Des-16	Jan-17	Badiliko la mwezi mmoja	Badiliko la miezi 12
1	Vyakula na vinywaji baridi	38.5	100.99	106.95	108.68	1.6	7.6
2	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	3.7	100.18	105.11	105.20	0.1	5.0
3	Mavazi ya nguo na viatu	8.3	100.90	103.72	104.35	0.6	3.4
4	Nishati, Maji na Makazi	11.6	101.63	109.93	111.27	1.2	9.5
5	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	6.3	100.53	103.98	103.86	-0.1	3.3
6	Gharama za Afya	2.9	100.49	104.72	105.28	0.5	4.8
7	Usafirishaji	12.5	99.66	100.32	100.27	0.0	0.6
8	Mawasiliano	5.6	99.98	99.09	99.11	0.0	-0.9
9	Utamaduni na Burudani	1.6	100.28	101.84	101.03	-0.8	0.7
10	Elimu	1.5	100.96	102.64	102.75	0.1	1.8
11	Hoteli na Migahawa	4.2	100.27	104.24	104.21	0.0	3.9
12	Bidhaa na huduma nyinginezo	3.1	100.62	102.86	102.93	0.1	2.3
<b>JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE</b>		<b>100.00</b>	<b>100.71</b>	<b>105.04</b>	<b>105.92</b>	<b>0.8</b>	<b>5.2</b>
<b>Makundi Mengine Teule</b>							
1	Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa nyumbani na mahotelini	37.07	101.07	107.44	109.31	1.7	8.2
2	Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika nyumbani pamoja na petroli na dizeli	8.68	101.38	111.66	113.05	1.2	11.5
3	Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula	62.93	100.50	103.77	104.12	0.3	3.6
4	Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta	54.25	100.35	102.51	102.69	0.2	2.3

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali Namba 1 hapo juu linaonesha kuwa, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwezi Januari, 2017 umeongezeka hadi kufikia asilimia 5.2 kutoka asilimia 5.0 mwezi Desemba, 2016. Hii inamaanisha kuwa, kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Januari, 2017 imeongezeka ikilinganishwa na kasi ya upandaji ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba, 2016. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 105.92 mwezi Januari, 2017 kutoka 100.71 mwezi Januari, 2016. Mfumuko wa Bei wa bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwezi Januari, 2017 umeongezeka hadi asilimia 7.6 kutoka asilimia 7.0 ilivyokuwa mwezi Desemba, 2016.

### **Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula**


Mfumuko wa Bei kwa kipimo cha mwaka wa bidhaa za vyakula nyumbani na migahawani kwa mwezi Januari, 2017 umeongezeka hadi asilimia 8.2 kutoka asilimia 7.4 mwezi Desemba, 2016. Aidha, badiliko la Fahirisi za Bei kwa bidhaa zisizo za vyakula limepungua hadi asilimia 3.6 mwezi Januari, 2017 kutoka asilimia 3.8 wa mwezi Desemba, 2016.

## Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi Januari, 2017 umepungua hadi asilimia 2.3 kutoka asilimia 2.5 ilivyokuwa mwezi Desemba, 2016.

Fahirisi inayotumika kukokotoa aina hii ya Mfumuko wa Bei, hajumuishi vyakula vinavyoliwa nyumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa, kuni na umeme. Vyakula na bidhaa za nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara, hivyo vikiondolewa kwenye fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

### Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Januari, 2016 hadi Januari, 2017. (Des., 2015 = 100)



Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonyesha kuwa, Fahirisi za Bei zimekuwa na mwenendo imara kutoka mwezi Januari, 2016 hadi mwezi Januari, 2017. Katika kipindi hicho, Mfumuko wa Bei nao umekuwa na mwenendo imara kutoka asilimia 6.5 mwezi Januari, 2016 hadi asilimia 5.2 mwezi Januari, 2017.

### MFUMUKO WA BEI WA MWEZI JANUARI, 2017 KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZAKA KWA ASILIMIA 0.8

Mfumuko wa Bei wa mwezi Januari, 2017 unaopimwa kwa kipimo cha mwezi umeongezaka kwa asilimia 0.8 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 0.7 ilivyokuwa mwezi Desemba, 2016. Fahirisi za Bei zimeongezaka hadi 105.92 mwezi Januari, 2017 kutoka 105.04 mwezi Desemba, 2016. Kuongezeka kwa Fahirisi za Bei kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi ni pamoja na mahindi kwa asilimia 16.0, unga wa mahindi kwa asilimia 10.0, mchele kwa asilimia 2.6, maharage kwa asilimia 6.3, ndizi za kupika kwa asilimia 5.8, magimbi kwa asilimia 5.3 na viazi vitamu kwa asilimia 2.5. Kwa upande mwagine, baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi ni pamoja na mkaa kwa asilimia 3.2 na majokofu kwa asilimia 2.4.


## **THAMANI YA SHILINGI YA TANZANIA MWEZI JANUARI, 2017 KUTOKA MWEZI DESEMBA, 2015**

Thamani ya Shilingi ya Tanzania hupima badiliko la Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma zilezile za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania ingeweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa Fahirisi za Bei za Taifa zinaongezeka, Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma hupungua.

Uwezo wa Shilingi 100 ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma umefikia Shilingi 94 na senti 42 mwezi Januari, 2017 ikilinganishwa na Shilingi 95 na senti 20 ilivyokuwa mwezi Desemba, 2016.

### **MIENENDO YA BEI**

#### **Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei Kutoka Mwezi Januari, 2016 hadi Januari, 2017. (Des., 2015 = 100)**



Kielelezo Namba 2 hapo juu kinaonesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya Fahirisi za Bei kuanzia mwezi Januari, 2016 hadi mwezi Januari, 2017. Kwa wastani, Fahirisi za nishati na mafuta na Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganishwa na fahirisi nyingine. Kundi la nishati na mafuta limeonesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo jumuisha chakula pamoja na nishati zimeonesha mwenendo wa bei ulio imara.

#### **Jedwali Namba 2: Shajala ya Fahirisi za Bei za Taifa kwa Miezi Ijayo**

Fahirisi za Bei za Taifa	Tarehe ya Toleo
Februari, 2017	08 Machi, 2016
Machi, 2017	10 Aprili, 2017
April, 2017	08 <sup>th</sup> Mei, 2017

**Mawasiliano:**

**Mkurugenzi Mkuu,  
Ofisi ya Taifa ya Takwimu**